

CHUO CHA MIPANGO YA MAENDELEO VIJIJINI DODOMA – TANZANIA



S.L.P. 138
DODOMA
Tanzania

Toleo Na 55

Simu: +255 262963037
Nukushi: +255 262963036
Barua Pepe: mpro@irdp.ac.tz
Tovuti: www.irdp.ac.tz

TAARIFA KWA UMMA

Mwanza, Ijumaa 04 Machi, 2022.

Hii ni kuwataarifu Wanajumuiya wa Chuo Cha Mipango ya Maendeleo Vijijini na Umma kwa ujumla, kuwa katika Kikao chake cha 124 kilichofanyika leo Ijumaa Machi 04, 2022 pamoja na mambo mengine Baraza la Uongozi wa Chuo limewateua watumishi wafuatao kushika nafasi mbali mbali kama ifuatavyo: -

1. Prof. Juvenal Nkonoki ameteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Kituo cha Mafunzo cha Kanda ya Ziwa – Mwanza. Kabla ya uteuzi huu Prof. Nkonoki alikuwa Kaimu Mkurugenzi wa Kituo cha Mafunzo cha Kanda ya Ziwa – Mwanza kutokana na nafasi hiyo kuwa wazi kufuatia kufariki Prof. Benedict Kilobe Mwezi Machi Mwaka 2020 aliyekuwa Mkurugenzi. Prof. Nkonoki atahudumu nafasi hii kwa kipindi cha Miaka minne;
2. Dkt. Godrick I. Mnyone ameteuliwa kuwa Mkuu wa Idara ya Mipango ya Mazingira kwa muda wa miaka mitatu. Dkt. Mnyone anatumikia cheo hiki kwa awamu ya pili sasa;
3. Dkt. Judith A. Namabira ameteuliwa kuwa Mkuu wa Idara ya Mafunzo ya Fedha za Maendeleo na Uongozi. Dkt. Namabira anachukua nafasi ya Prof. Zacharia Masanyiwa ambae amemaliza muda wake wa vipindi viwili vya Ukuu wa Idara;
4. Dkt. Maseke R. Mgabo ameteuliwa kuwa Mkuu wa Idara ya Mafunzo ya Idadi ya Watu ambae anachukua nafasi iliyoachwa wazi na Prof. John Safari ambae aliteuliwa kuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo -Taaluma wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MOCU); na
5. Dkt. Hosea A. Mpogole ameteuliwa kuwa Mkuu wa Idara ya Utafiti na Uelekezi. Kabla ya uteuzi huu Dkt. Mpogole alikuwa Kaimu Mkuu wa Idara ya Utafiti na Uelekezi kufuatia aliyekuwa Mkuu wa Idara hii Prof. James Lweramila kufariki Mwezi Machi Mwaka 2021.

Uteuzi huu unaanza leo Ijumaa tarehe 04 Machi, 2022.

Imetolewa na,

Godrick H.B. Ngolly

Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Uhusiano